JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI

# MWONGOZO WA UENDESHAJI WA VITUO ATAMIZI VYA UFUGAJI MIFUGO KIBIASHARA KWA VIJANA NCHINI



Septemba, 2022 | Toleo la Kwanza

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI

# MWONGOZO WA UENDESHAJI WA VITUO ATAMIZI VYA UFUGAJI MIFUGO KIBIASHARA KWA VIJANA NCHINI

**Septemba, 2022 | Toleo la Kwanza**

## DIBAJI

Mwongozo wa Uanzishaji na Uendeshaji wa Vituo Atamizi vya Ufugaji Mifugo Kibiashara kwa Vijana nchini umeandaliwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa ajili ya kusimamia uanzishaji na uendeshaji wa Vituo husika katika taasisi za Serikali na Sekta binafsi.

Lengo la mwongozo huu ni kutoa utaratibu kwa watendaji ili waweze kusimamia uanzishaji na uendeshaji wa Vituo Atamizi vitakavyotumika kuwawezesha vijana kupata ujuzi, uzoefu na ujasiri katika kuanzisha miradi ya ufugaji yenye tija na ya kibiashara. Kwa muktadha huo, mpango huu unalenga kuongeza fursa za ajira nchini, kujiongezea kipato, kuongeza mchango wa Sekta ya Mifugo kwenye pato la Taifa, na kuongeza upatikanaji wa mifugo bora kwa ajili ya soko la ndani na nje ya nchi

Mwongozo huu umebainisha mambo muhimu ikiwemo umuhimu, malengo, mahitaji kwa ajili ya uanzishaji na uendeshaji wa Vituo Atamizi vya ufugaji wa mifugo kibiashara, pamoja na kuainisha majukumu ya wadau muhimu watakaoshiriki katika uanzishaji na uendeshaji wa Vituo tarajiwa.

Wizara ya Mifugo na Uvuvi inatarajia kuona Mwongozo huu ukitumiwa na wadau mbalimbali katika mnyororo wa Sekta ya Mifugo wakiwemo sekta binafsi, taasisi za umma, mashirika ya dini, mashirika yasiyo ya serikali (NGOs), Asasi za kiraia, Taasisi za fedha na wabia wa maendeleo ili kuunga mkono juhudi za serikali katika kutatua changamoto kubwa ya ajira kwa vijana pamoja na kuchangia katika kuleta mageuzi ya sekta ya mifugo nchini.

**Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki (Mb)**

Waziri wa Mifugo na Uvuvi

## SHUKRANI

Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Sekta ya Mifugo) anatoa shukrani za dhati kwa Wakala ya Mafunzo ya Mifugo (LITA) na Taasisi ya Utafiti wa Mifugo (TALIRI) pamoja na Menejimenti ya Wizara kwa kuweza kufanikisha maandalizi ya Mwongozo huu.

Shukrani ziende kwa Menejimenti ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kwa kutoa ushauri elekezi wa namna ya kuandaa na kutekeleza miradi ya Vituo Atamizi kwa vijana. Ni kupitia uzoefu wao, tumeweza kukamilisha maandalizi ya utekelezaji wa Vituo Atamizi kwa muda mfupi kuliko ilivyotarajiwa. Aidha, shukrani za pekee ziwaendee vijana wa SUGGECO kwa wasilisho na taarifa yao ya uzoefu katika uendeshaji wa Vituo Atamizi ambayo ilisaidia kwa kiwango kikubwa wakati wa uandaaji wa Mwongozo huu.

Pia, tunawashukuru wataalamu mbalimbali waliohusika katika uandishi na kuhariri andiko hili hadi kukamilika kwake. Kwa upekee kabisa nawashukuru Dkt. Pius L. Mwambene (Mtendaji Mkuu - LITA), Dkt. Angello J. Mwilawa (Mkurugenzi Idara ya Utafiti, Mafunzo na Huduma

za Ugani), Profesa Erick Vitus Komba (Mkurugenzi Mkuu - TALIRI), Dkt Hassan Mrutu (Mkurugenzi Msaidizi Utafiti, Mafunzo na Ugani), Bw. Joseph L. Msemwa (Mkuu wa Idara ya Utafiti na Ushauri - LITA), Bw. Hosea Kimata (Mkufunzi Mwandamizi - LITA), Dkt. Jonas B. Kizima (Mtafiti Mkuu - TALIRI), Bw. Bernad M. Francis (Mchumi - TALIRI), Bw. Tumsime L. Mutta (Mchumi - TALIRI) na Dkt. Bertha Dugange (Mratibu wa Sekta ya Mifugo kutoka OR-TAMISEMI).

**Bw. Tixon T. Nzunda**

Katibu Mkuu,

Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Sekta ya Mifugo)

**YALIYOMO**

**DIBAJI……………………………………………………………i**

**SHUKRANI………………………………………………………iii**

**1.0 UTANGULIZI…………………………………………………1**

1.1 Maana ya Vituo Atamizi vya Ufugaji kwa Vijana……….2

1.2 Umuhimu wa Vituo Atamizi vya Ufugaji Mifugo Kibiashara kwa Vijana ………………….…………………… 3

1.2.1 Lengo kuu……………………………………….…………..5

1.2.2 Malengo mahsusi………………………………………….5

**2.0 MFUMO WA UENDESHAJI MIRADI YA VITUO ATAMIZI…………………………………………………………...7**

**3.0 UENDESHAJI WA VITUO ATAMIZI………………..10**

3.1 Usajili wa washiriki………..…………………….........10

3.2 Utekelezaji wa Vituo Atamizi……………………..………12

3.2.1 Kuwajengea uwezo washiriki………………………....13

3.2.2 Kuwajengea uwezo walezi/wasimamizi ..…..………13

3.2.3 Uanzishaji na uendeshaji wa miradi ya ufugaji mifugo kibiashara……………………………………………………...14

3.2.4 Wadau muhimu watakaoshiriki katika utekelezaji wa miradi ya ufugaji mifugo kibiashara kupitia vituo atamizi pamoja na majukumu yao……………..……………….15

3.2.5 Mtiririko wa uanzishaji na uendeshaji wa Vituo Atamizi....................................................................19

3.2.6 Mtindo wa Uendeshaji Vituo Atamizi……..…..……...26

**4.0 MATOKEO TARAJIWA……………………………...27**

**5.0 UFUATILIAJI NA THATHIMINI……………………..28**

5.1 Faida ya ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya ufugaji mifugo kibiashara……..................................................................29

5.2 Mambo yatakayozingatiwa wakati wa ufuatiliaji wa Miradi ya ufugaji mifugo kibiashara………………………..29

5.3 Vielelezo vitakavyotumika kukusanyia taarifa wakati wa ufuatiliaji wa miradi katika vituo Atamaizi………………..…...30

**6.0 HITIMISHO……………………………………………31**

## 1.0 UTANGULIZI

Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Sekta ya Mifugo imeendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji hasa katika tasnia ya nyama. Msukumo huu umesababisha ongezeko la uwekezaji katika machinjio na viwanda vikubwa vya kusindika nyama nchini sanjari na ongezeko la mahitaji ya mifugo bora ya kuchinja. Ongezeko la mahitaji ya mifugo bora limeendelea kutofikiwa kutokana na sehemu kubwa ya ufugaji hapa nchini kuwa katika mifumo ya asili isiyokuwa ya kibiashara.

Ili kukidhi mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi linaloendelea kukua, hatua za makusudi zinahitajika kuchukuliwa kwa ajili ya kuboresha mfumo wa asili wa ufugaji mifugo nchini kuwa wa kibiashara. Maboresho hayo pia yanahitaji mabadiliko ya kifikra ya wafugaji na wadau wengine katika sekta ya mifugo sanjari na kuandaa wafugaji watakaofuga kibiashara ili kuongeza upatikanaji wa mifugo bora, fursa za ajira na kipato cha kaya na taifa kwa ujumla.

Uwepo wa wahitimu wengi wa fani za mifugo nchini wasiokuwa na ajira rasmi unaweza kuwa chachu ya

mabadiliko katika sekta ya mifugo endapo wataandaliwa na kuwezeshwa kuwa wafugaji wa kibiashara. Uwezeshwaji huo pia utasaidia kuongeza fursa za ajira kwa vijana ambao ndio nguvu kazi tarajiwa katika jamii ya kitanzania.

Mafunzo ya ufugaji wenye tija kupitia Vituo Atamizi yanaweza kutumika kuwajengea uwezo na ujasiri wa kuanzisha na kuendesha miradi ya uzalishaji wa mifugo bora kibiashara. Uanzishaji na uendeshaji wa Vituo Atamizi kwa ajili ya ufugaji wa kibiashara ikiwemo unenepeshaji ng'ombe bora wa nyama kwa vijana ni njia mojawapo inayoweza kusaidia kukidhi mahitaji ya soko la mifugo hai na nyama bora ndani na nje ya nchi. Utaratibu huu pia ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango wa Mabadiliko ya Sekta ya Mifugo katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2022/2023 – 2026/2027).

## 1.1 Maana ya Vituo Atamizi vya ufugaji kwa vijana

Vituo Atamizi ni utaratibu wa muda maalum (kati ya mwaka mmoja hadi miwili) wa kuwalea na kuwajengea uwezo na ujasiri vijana kutumia stadi mbalimbali wanazopatiwa ili kubuni na kutekeleza miradi ya kibiashara. Lengo la utaratibu wa Vituo Atamizi ni kumuwezesha mshiriki

kuwekeza na kuendesha miradi husika kwa mafanikio baada ya kupata uzoefu na mafunzo ya ujuzi na ujasiriamali kupitia Vituo hivyo.

Kwa muktadha wa Sekta ya mifugo, uwepo wa Vituo Atamizi unalenga kuwalea vijana na kuwajengea uwezo wa kutumia stadi rahisi za kuanzisha na kuendeleza miradi ya uzalishaji wa mifugo bora kibiashara ikiwemo miradi ya unenepeshaji.

## 1.2 Umuhimu wa Vituo Atamizi vya ufugaji mifugo kibiashara kwa vijana

Hapa duniani, karibu robo tatu ya vijana wenye umri kati ya miaka 18 hadi 30 hawana ajira rasmi ukilinganisha na watu wazima. Vijana zaidi ya milioni 75 duniani wamehitimu mafunzo mbalimbali lakini hawana ajira rasmi. Katika kipindi cha miaka 10 ijayo, vijana zaidi ya bilioni moja wanategemewa kuhitimu mafunzo mbalimbali na kuingia kwenye soko la ajira. Kwa upande wa Tanzania, vijana takriban milioni moja huhitimu mafunzo mbalimbali kila mwaka lakini wanaopata ajira katika sekta ya umma ni takriban elfu 40 na sekta binafsi ni 350,000. Kwa upande wa sekta ya mifugo, vijana takriban 1,600 huhitimu mafunzo

ya mifugo katika ngazi ya astashahada, stashahada na shahada kila mwaka ambapo ni asilimia 9.5 pekee ndiyo wanaobahatika kuingia kwenye ajira rasmi (Mlozi, 2020).

Kwa upande mwingine, upatikanaji wa mifugo bora kama malighafi kwa ajili ya viwanda vya nyama hapa nchini, takwimu zinaonesha kuwepo kwa upungufu mkubwa wa mifugo bora usioendana na uwezo wa usimikaji wa viwanda vya nyama vilivyopo. Kwa mfano, kiwanda cha Tan Choice kilichopo Kibaha mkoani Pwani kina uwezo wa kuchinja ng'ombe 1,000 kwa siku lakini ng'ombe wanaopatikana hawazidi asilimia 30 ya idadi hiyo. Aidha, kiwanda hicho kina uwezo wa kuchinja mbuzi na kondoo 1,500 kwa siku lakini wanaopatikana ni asilimia 67 pekee.

Kwa hiyo, wahitimu wengi katika fani za mifugo wasiokuwa na ajira rasmi wanaweza kutumia fursa ya uwepo wa mahitaji makubwa ya mifugo bora kwa kuingia kwenye uzalishaji kibiashara ili kusaidia kuhamasisha ufugaji wenye tija, kukidhi mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi, kuongeza fursa za ajira na hatimaye kuongeza kipato cha kaya na taifa.

Pamoja na uwepo wa vijana wengi wakiwemo wahitimu wa fani za mifugo, imebainika kuwa wengi wao hushindwa kuanzisha miradi ya uzalishaji yenye tija kutokana na kukosa stadi za ufugaji kibiashara, uwezo wa kupata ardhi, uwezo wa kupata mitaji, na uwezo wa kupata taarifa za masoko. Hivyo, Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi, imekusudia kuanzisha na kuendesha Vituo Atamizi vya ufugaji mifugo kibiashara kwa kuanza na vijana wahitimu wa fani za mifugo katika ngazi za astashahada, stashahada na shahada kwa malengo yafuatayo:-

### 1.2.1 Lengo kuu

Lengo la mwongozo huu ni kutoa utaratibu kwa watendaji ili waweze kusimamia uanzishaji na uendeshaji wa Vituo Atamizi vitakavyotumika kuwawezesha vijana kupata ujuzi, uzoefu na ujasiri katika kuanzisha miradi ya ufugaji yenye tija na ya kibiashara. Vituo hivi vitatumika kuwaandaa vijana kuingia kwenye ufugaji wenye tija na wa kibiashara ili kuongeza fursa za ajira, kujiongezea kipato, kuongeza mchango wa sekta ya mifugo kwenye pato la taifa, na kuongeza upatikanaji wa mifugo bora kwa ajili ya soko la ndani na nje ya nchi.

### 1.2.2 Malengo mahsusi

i. Kuwawezesha vijana kuanzisha na kuendesha miradi ya ufugaji wa mifugo kibiashara;
ii. Kuwapatia vijana stadi rahisi kwa vitendo za namna bora ya kuanzisha na kuwekeza katika miradi ya ufugaji wa mifugo kibiashara;
iii. Kuwawezesha vijana kupata ujuzi, uzoefu na ujasiri wa kuanzisha miradi ya ufugaji kibiashara
iv. Kuhamasisha vijana kuunda vikundi vya ushirika; na
v. Kuwaunganisha vijana na wadau mbalimbali kwenye mnyororo wa thamani wa uzalishaji mifugo kibiashara.

## 2.0 MFUMO WA UENDESHAJI MIRADI YA UFUGAJI KIBIASHARA KATIKA VITUO ATAMIZI

Mfumo wa uendeshaji mafunzo ya ufugaji kibiashara katika Vituo Atamizi utashirikisha Vijana washiriki; Wakufunzi; Walezi, Wafanyabiashara; Wasindikaji; Watoa huduma za vyakula vya mifugo na dawa; Serikali za mitaa; Taasisi za fedha; Mamlaka za udhibiti ubora na usajili wa biashara; Asasi za kiraia; na Vyuo. Mfumo huu shirikishi utazingatia mambo yafuatayo:-

i. Uanzishwaji wa Vituo Atamizi vyenye miundombinu muhimu ya ufugaji kibiashara ikiwemo banda la kunenepeshea, josho, vyanzo vya maji, mabirika ya kunyweshea maji, mizani, kibanio, eneo la kupakilia na kushushia mifugo, eneo la malisho, zizi, pamoja na zana za kuzalishia malisho;

ii. Kuwepo kwa vijana wasiozidi 30 kwa kila kituo watakaokidhi vigezo vilivyowekwa;

iii. Kuwepo kwa fedha za kuwezesha kuanzisha na kuendesha Vituo Atamizi kwa kuzingatia utaratibu ufuatao:-

    a) Kuwa na mtaji wa kuanzia;
    b) Kufungua akaunti ya benki;

c) Kuwa na utaratibu wa utoaji na matumizi ya fedha kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za matumizi ya fedha;

d) Kuanzisha ushirika wa washiriki wa ufugaji wa mifugo katika kituo Atamizi utakaowawezesha kuanzisha SACCOS au AMCOS baada ya kutoka kwenye Vituo Atamizi;

e) Kukokotoa faida ambayo sehemu yake itakuwa ni mtaji wa washiriki baada ya kuhitimu.

iv. Taasisi zitakazoendesha Vituo Atamizi zitawaunganisha vijana watakaohitimu mafunzo tarajiwa na walezi wafuatao:-

a) Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa ajili ya kufanya tathimini; kuwawezesha na kuwalea kama wawekezaji; pamoja na kuwaunganisha na masoko;

b) Sekretarieti za Mikoa na mamlaka za serikali za mitaa kwa ajili ya kupatiwa maeneo ya uwekezaji pamoja na mikopo ikiwemo 4% ya mikopo kwa vijana;

c) Taasisi za kifedha na Wadau wa maendeleo kwa ajili ya kuwaonesha fursa za mikopo na ufadhili wa kuendelea na miradi ya ufugaji wa

mifugo kibiashara mara baada ya kumaliza kipindi cha uAtamizi.

## 3.0 UENDESHAJI WA VITUO ATAMIZI

Uendeshaji wa Vituo Atamizi utahusisha usajili wa washiriki kwa kuzingatia sifa stahiki na utekelezaji shirikishi wa miradi.

### 3.1 Usajili wa washiriki

i) Nafasi za ushiriki zitatangazwa kupitia vyombo mbalimbali vya habari;

ii) Washiriki watatakiwa kutuma maombi kwenye kituo husika;

iii) Uchambuzi wa maombi utafanyika kwa hatua mbili ili kuwapata washiriki stahiki kulingana na sifa na vigezo vilivyowekwa; na

iv) Waombaji watakaochaguliwa katika hatua ya kwanza watapewa taarifa na utaratibu wa kufika Vituoni kwa ajili ya hatua ya pili ya usaili.

**Sifa za kusajiliwa**

Mpango huu unalenga kuwafikia vijana wa kike na wa kiume watakaoomba kushiriki kwa kuzingatia sifa zifuatazo:-

i. Awe raia wa Tanzania

ii. Mhitimu wa elimu ya msingi, astashahada, stashahada au shahada ya mifugo katika vyuo vinavyotambulika na serikali;
iii. Mwenye umri wa miaka 18 - 30;

**Masharti kwa washiriki katika Vituo Atamizi**

Kila mshiriki atakayekuwa tayari kujiunga katika Vituo Atamizi atalazimika kukubali na kufuata masharti yafuatayo:-

i. Awe na mdhamini mwenye kitambulisho cha taifa;
ii. Awe tayari kuishi katika kituo Atamizi wakati wa utekelezaji wa mradi;
iii. Awe tayari kushiriki mafunzo katika kipindi maalum cha mradi husika kilichopangwa bila kukatisha;
iv. Awe tayari kutii sheria za nchi na mamlaka;
v. Awe tayari kutii kanuni, miongozo na taratibu za uendeshaji wa kituo husika;
vi. Awe na afya njema itakayomuwezesha kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa kazi za mradi;
vii. Awe tayari kuridhia kuacha mgao wake wa faida ya mradi mpaka mwisho wa mradi;
viii. Awe tayari kujitolea na kujifunza ujasiriamali;

ix. Awe tayari kuishi katika kituo Atamizi atakachopangiwa wakati wote wa utekelezaji wa mradi;
x. Awe tayari kusimamia, kutunza na kulinda mali za mradi; na
xi. Mwombaji wawe tayari kujigharamia nauli, malazi na chakula wakati wa usaili wa ana kwa ana Vituoni ndani ya siku saba.

## 3.2 Utekelezaji wa Vituo Atamizi

Utekelezaji wa Vituo Atamizi utaanza na Mafunzo kwa wasimamizi na washiriki yatakayofuatiwa na uanzishaji na uendeshaji wa miradi ya uzalishaji kibiashara, kama ifuatavyo:-

### 3.2.1 Kuwajengea uwezo washiriki

Washiriki watajengewa uwezo katika maeneo yafuatayo:-

i. Stadi na hamasa ya mabadiliko kifikra na mtazamo chanya;
ii. Teknolojia sahihi za ufugaji mifugo kibiashara;
iii. Teknolojia sahihi za uzalishaji wa malisho na mbegu za malisho;

iv. Mahitaji muhimu yanayotakiwa katika uzalishaji ikiwemo teknolojia ya uchanganyaji wa vyakula na ulishaji;
v. Stadi za biashara na uandishi wa mipango biashara yenye sifa za kukopesheka;
vi. Mbinu za utafutaji wa masoko;
vii. Utunzaji wa kumbukumbu na hesabu za fedha;
viii. Kutambua na kutumia fursa mbalimbali za mikopo;
ix. Kutengeneza mtandao (networking) wa kuwasiliana na wadau muhimu katika mnyororo wa thamani wa uzalishaji mifugo;
x. Sheria, Kanuni, Miongozo na Taratibu za uendeshaji biashara ya mifugo hai na mazao yake; na
xi. Kuunda na kuendesha vikundi vya ushirika.

### 3.2.2 Kuwajengea uwezo wasimamizi/walezi (mentors) wa Vituo

Wasimamizi/walezi wa Vituo watajengewa uwezo katika maeneo yafuatayo:-

i. Uwezo wa kuchambua na kutambua washiriki wenye sifa stahiki watakaokuwa tayari kushiriki kikamilifu katika mafunzo na uendeshaji wa miradi tarajiwa

ii. Mbinu, ujuzi na uzoefu katika ulezi na utoaji hamasa ya mabadiliko ya kifikra na mtazamo chanya kwa washiriki;
iii. Usimamizi na ufuatiliaji wa karibu wa ushiriki na uwajibikaji wa washiriki;
iv. Usimamizi, usaidizi na ushauri kwa washiriki wakati wa uandishi wa mipango biashara, manunuzi, matumizi ya fedha za miradi, uendeshaji, utunzaji kumbukumbu na biashara za mradi; na
v. Uandaaji wa taarifa za utekelezaji na kuziwasilisha katika ngazi za juu

### 3.2.3 Uanzishaji na uendeshaji wa miradi ya ufugaji mifugo kibiashara

Washiriki wataanzisha na kuendesha miradi ya ufugaji wa mifugo kwa tija kwa kuzingatia miongozo/mikakati iliyoainishwa katika mipango biashara chini ya uangalizi wa wasimamizi/wakufunzi. Washiriki watawezeshwa kujikimu ili kuweza kushiriki ipasavyo. Katika utekelezaji wa miradi hiyo ya ufugaji wa mifugo kibiashara, Vituo Atamizi vitaanza na teknolojia ya unenepeshaji kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya malighafi ya viwanda vya nyama. Vyanzo vya upatikanaji

wa mifugo kwa ajili ya miradi ya unenepeshaji vitajumuisha minada ya mifugo na wafugaji binafsi.

### 3.2.4 Wadau muhimu watakaoshiriki katika utekelezaji wa miradi ya ufugaji mifugo kibiashara kupitia vituo atamizi pamoja na majukumu yao

Wadau muhimu watakaoshirikishwa katika utekelezaji wa miradi ya ufugaji mifugo kibiashara kupitia Vituo Atamizi pamoja na majukumu yao ni kama ilivyoainishwa hapa chini:-

**Wizara ya Mifugo na Uvuvi**

Majukumu ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi yatakuwa kama ifuatavyo:

i. Kuwezesha upatikanaji wa rasilimali fedha;
ii. Kuandaa na kuratibu utekelezaji wa mwongozo wa unenepeshaji wa mifugo kwa ajili ya nyama;
iii. Kuratibu uendeshaji wa Vituo Atamizi kupitia Idara ya Utafiti, Mafunzo na huduma za Ugani; na
iv. Kufanya ufuatiliaji na tathmini.

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI)**

Majukumu ya OR-TAMISEMI yatakuwa kama ifuatavyo:

i. Kuwa kiungo kati ya Wizara na Tawala za Mikoa katika kufanikisha utekelezaji wa maelekezo kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuhusu Uendeshaji wa Vituo Atamizi
ii. Kutoa mwongozo na ushauri kwa Mikoa katika mambo ya kisheria na utaratibu kuhusu Uendeshaji wa Vituo Atamizi
iii. Kuweka mazingira wezeshi kwa Vituo Atamizi kuweza kufanya kazi katika Mikoa na Halmashauri
iv. Kushirikiana na timu za Wizara ya Mifugo na Uvuvi katika kuratibu, kushauri, kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa shughuli zinazoendeshwa na Vituo Atamizi katika Mikoa na Halmashauri

**Ofisi za Mikoa (Regional Secretariat)**

Majukumu ya Ofisi za Mikoa yatakuwa kama ifuatavyo:

i. Kuzielekeza na kuzisimamia Mamlaka za Serikali za Mitaa kutekeleza maelekezo kutoka OR -TAMISEMI kuhusu Uendeshaji wa Vituo Atamizi
ii. Kushirikiana na timu za Wizara ya Mifugo na Uvuvi na OR-TAMISEMI kufuatilia na kutathmini

Uendeshaji wa Vituo Atamizi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa

**Mamlaka za Serikali za Mitaa (MSM)**

Majukumu ya MSM yatakuwa kama ifuatavyo:

i. Kutekeleza maelekezo kutoka Sekretarieti za Mikoa kuhusu Uendeshaji wa Vituo Atamizi
ii. Kushirikiana na timu za Wizara ya Mifugo na Uvuvi, OR-TAMISEMI na Sekretatarieti za Mikoa katika kufuatilia Uendeshaji wa Vituo Atamizi
iii. Kusaidia upatikanaji wa fursa na rasilimali mbalimbali za ufugaji kibiashara kwa vijana baada ya kumaliza mafunzo kupitia Vituo Atamizi;
iv. Kusaidia upatikanaji wa taarifa za masoko na bei za bidhaa;
v. Kusaidia upatikanaji wa taarifa za washiriki wakati wa usaili;
vi. Kusaidia upatikanaji wa mikopo yenye riba nafuu kwa washiriki; na
vii. Kusaidia upatikanaji wa maeneo ya uwekezaji.

**Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu**

Majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu yatakuwa kama ifuatavyo:

i. Kusaidia ufadhili kwa vijana wanaojiunga na Vituo Atamizi;
ii. Kushiriki katika kutoa mafunzo elekezi ya ujasiriamali na uwekezaji kibiashara;
iii. Kuwa mshauri na kiungo kwa vijana na fursa za ajira; na
iv. Kuwaunganisha wahitimu na Baraza la Taifa la uwezeshaji wananchi kiuchumi
v. Kushirikiana na timu za Wizara ya Mifugo na Uvuvi, OR-TAMISEMI na Sekretatarieti za Mikoa katika kufuatilia na kutathmini Uendeshaji wa Vituo Atamizi

**Washiriki (incubatees)**

Washiriki wa mradi huu watakkuwa na majukumu yafuatayo:

i. Kuandaa mpango biashara wa ufugaji mifugo kwa kushirikiana na wakufunzi;
ii. Kuandaa miundombinu ya ufugaji/unenepeshaji mifugo wa nyama, ikiwemo uzalishaji wa malisho;

iii. Kutafuta na kununua mahitaji ya mradi kwa kuzingatia mpango biashara husika ikiwemo ununuzi wa mifugo, vyakula, madawa na vitendea kazi kwa kushirikiana na wakufunzi;
iv. Kutekeleza shughuli za kila siku za mradi kama ilivyoainishwa katika mpango biashara husika;
v. Kutafuta masoko na kufanya biashara ya mifugo kwa ajili ya nyama; na
vi. Kusimamia, kutunza na kulinda mradi.

**Taasisi Watekelezaji wa Mradi (TALIRI, LITA na Wadau wengine watakaojitokeza)**

i. Kusajili washiriki;
ii. Kuwezesha upatikanaji wa rasilimali muhimu za uendeshaji wa miradi;
iii. Kuandaa viashiria vya kupima utendaji na ufanisi wa miradi;
iv. Kujenga miundombinu muhimu ya miradi ikiwemo uzalishaji wa malisho;
v. Kusimamia utaratibu mzima wa uendeshaji wa Vituo;
vi. Kuwajengea uwezo wasimamizi/walezi wa vituo;
vii. Kuwajengea uwezo washiriki kwenye Vituo Atamizi;

viii. Kushirikiana na Wizara katika kufanya ufuatiliaji na tathmini;

ix. Kuwaunganisha washiriki na Taasisi za fedha, sekretariati za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, viwanda, makampuni ya kununua mifugo walionenepeshwa na wadau wengine wa maendeleo; na

x. Kuandaa taarifa za utekelezaji na kuwasilisha Wizarani kila mara.

**Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO)**

i. Kuandaa vitalu vyenye miundombinu muhimu kwa ajili ya kukodisha kwa wafanyabiashara wahitimu kutoka kwenye Vituo Atamizi;

ii. Kuwapa mafunzo elekezi ya ufugaji kwenye maeneo husika;

iii. Kuwapangisha vikundi vya vijana waliomaliza mafunzo kutoka Vituo Atamizi maeneo ya kufugia kwa kuzingatia masharti yatakayowekwa; na

iv. Kununua mifugo iliyonenepeshwa kutoka kwa vikundi vya vijana kwa ajili ya kuchinja na kuuza nyama bora kwenye bucha za kampuni

**Sekta binafsi**

i. Kuandaa maeneo yenye miundombinu muhimu kwa ajili ya kukodisha kwa wafanyabiashara wahitimu kutoka kwenye Vituo Atamizi;
ii. Kuwapa mafunzo elekezi ya ufugaji kwenye eneo husika; na
iii. Kuwapangisha vikundi vya vijana waliomaliza Vituo Atamizi maeneo ya kufugia kwa kuzingatia masharti yatakayowekwa.

**Taasisi za fedha**

i. Kutoa ushauri na mafunzo juu ya fursa mbalimbali za mikopo na namna ya kutekeleza mipango biashara katika kuanzisha na/au kuendeleza biashara zao pindi watakapomaliza muda wao wa kulelewa katika Vituo Atamizi; na
ii. Kusaidia kutoa mafunzo ya namna ya kutunza hesabu na fedha.

**Taasisi za Utafiti na Mafunzo**

i. Kufanya tafiti shirikishi na tumizi ili kupata teknolojia sahihi na rahisi kwa ajili ya uendeshaji wa miradi ya ufugaji kibiashara yenye tija

ii. Kushiriki kutoa mafunzo kwa washiriki na wasimamizi katika kipindi cha utekelezaji wa miradi ili kuwapa elimu na uzoefu wa maeneo mbalimbali katika sekta; na
iii. Kusaidia kuainisha viwango vya ubora wa mifugo walionenepeshwa na mahitaji ya soko ili kuwasaidia vijana kuzalisha kulingana na mahitaji ya soko.

**Wadau wengine (**viwanda, wafanyabiashara, wauza pembejeo na Asasi za kiraia**)**

i. Kubainisha fursa za masoko ya mifugo na mazao yake;
ii. Kuwauzia washiriki pembejeo mbalimbali zinazohitajika kwenye miradi;
iii. Vyanzo vya taarifa mbalimbali za mradi;
iv. Kushiriki kutoa mafunzo kwa washiriki katika kipindi cha utekelezaji wa miradi ili kuwapa uzoefu wa maeneo mbalimbali katika sekta; na
v. Kusaidia kuainisha viwango vya ubora wa mifugo walionenepeshwa na mahitaji ya soko ili kuwasaidia vijana kuzalisha kulingana na mahitaji ya soko.

### 3.2.5 Mtiririko wa uanzishaji na uendeshaji wa Vituo Atamizi

Uanzishaji na uendeshaji wa Vituo Atamizi utakuwa katika mtiririko wa hatua (phases) tatu, kama ifuatavyo:

**Hatua ya kwanza (pre-incubation) –** hatua hii itahusisha uandaaji wa mwongozo; upembuzi yakinifu utakaoshirikisha wadau muhimu; mafunzo kwa wasimamizi/walezi (mentors) wa Vituo ili kuwajengea uwezo wa kuweza kusimamia na kulea washiriki pamoja na utafutaji wa rasilimali fedha. Wadau muhimu watakaohusishwa katika hatua hii ni pamoja na wateja tarajiwa, wauzaji pembejeo, wauzaji wa mifugo, taasisi za fedha, mamlaka za serikali za mitaa, asasi za kiraia na wabia wa maendeleo. Wadau hawa watahusishwa katika kupata taarifa za masoko, pembejeo, utaalam, mitaji na taratibu za kisheria za uendeshaji wa biashara. Kwa upande mwingine, wadau watapata kuona fursa za kibiashara na masoko kutoka katika Vituo Atamizi. Hivyo, kutakuwa na mawasiliano ya pande zote mbili ili kufanikisha utekelezaji wa miradi kibiashara.

**Hatua ya pili (incubation)** - Utekelezaji wa hatua hii utaanza na usajili wa washiriki kwa kuzingatia sifa na

vigezo vilivyowekwa. Baada ya usajili, washiriki watashirikiana na wakufunzi kuibua mawazo ya kibiashara. Katika hatua hii, washiriki watatekeleza miradi biashara iliyopitishwa. Utekelezaji huo utahusisha ujenzi wa miundombinu ya mifugo; ununuzi wa mifugo, pembejeo na vitendea kazi; utendaji wa kazi za kila siku za shamba kama vile ulishaji, usafi, utoaji chanjo na tiba; utafutaji masoko na utunzaji wa kumbukumbu. Mbinu bora za ufugaji, uzalishaji malisho na ujasiriamali zitazingatiwa wakati wa utekelezaji. Kama ilivyokuwa katika hatua ya kwanza, hatua hii pia itawahusisha wadau muhimu waliotajwa hapo juu. Hatua hii itasaidia kuwaongezea washiriki ujuzi na ujasiri na hatimaye kuwaunganisha na washirika muhimu katika maisha yao baada ya kuhitimu mafunzo tarajiwa.

Katika hatua hii, washiriki pia wataandaliwa kuhusu namna bora ya kwenda kujitegemea mara baada ya kumaliza muda wao. Maandalizi hayo yatajumuisha:-


i. Kuandaa andiko la biashara lililokidhi sifa na vigezo litakalotekelezwa na wanufaika (mmoja mmoja au kikundi) mara baada ya kuhitimu;

ii. Washiriki kuunganishwa na wadau mbalimbali katika mnyororo wa thamani (masoko, taasisi za fedha, wauzaji pembejeo, mamlaka za serikali za mitaa, taasisi za ushauri, n.k.);
iii. Washiriki kupatiwa faida itakayotokana na miradi itakayotekelezwa katika Vituo Atamizi vilivyokubalika. Fedha hiyo itakuwa sehemu ya mtaji kwa ajili ya kwenda kuanzisha biashara zao kupitia vikundi au mnufaika mmoja mmoja;
iv. Washiriki kupewa vyeti vya ushiriki ili kuwarahisisishia kupata huduma na msaada utakaohitajika; na
v. Washiriki kujengewa uwezo na kuhamasishwa kuanzisha na kusajili vikundi vya ushirika.

**Hatua ya tatu (post-incubation)**

Katika hatua hii, washiriki wataunganishwa na walezi ambao ni pamoja na NARCO, Taasisi za fedha, Sekta binafsi, Wadau wa maendeleo na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kurahisisha uanzishaji, uwekezaji na uendeshaji wa miradi ya ufugaji wa mifugo kibiashara.

### 3.2.6 Mtindo wa Uendeshaji Vituo Atamizi



## 4 MATOKEO TARAJIWA

Kutokana na utekelezaji wa Vituo Atamizi vya unenepeshaji mifugo kwa ajili ya nyama hapa nchini, matokeo yafuatayo yanatarajiwa:-

i) Kuwa na vijana wanaojishughulisha na ufugaji mifugo kibiashara ikiwemo unenepeshaji wa mifugo;
ii) Kuongeza fursa za ajira;
iii) Kukua kwa biashara ya mifugo wa nyama walionenepeshwa;
iv) Kuongezeka kwa uzalishaji wa mifugo wa nyama wenye tija na hivyo kuongeza kipato cha washiriki na pato la Taifa; na
v) Kuongezeka kwa upatikanaji wa malighafi bora zitakazotumika kwenye viwanda vya kuchakata na kusindika nyama.

## 5.0 UFUATILIAJI NA TATHMINI

Ufuatiliaji na tathmini ni jukumu muhimu katika kuboresha mbinu na mikakati ya taasisi kufikia malengo na kutoa huduma stahiki kwa wananchi na wadau wote. Wakati wa utekelezaji wa miradi ya ufugaji mifugo kibiashara kupitia vituo atamizi, kutakuwa na zoezi la **ufuatiliaji** na **tathmini** ya miradi yote itakayotekelezwa litakalofanywa na timu ya nje.

Zoezi la ufuatiliaji litahusu ukusanyaji wa taarifa za utekelezaji wa viashiria na vigezo vya utekelezaji ili kuijulisha Menejimenti na wadau wengine juu ya hatua za utekelezaji zilizofikiwa katika kutimiza malengo na majukumu ambayo yametengewa fedha. Aidha, zoezi la **tathmini** litahusu uchambuzi wa maendeleo ya mradi ambapo muundo, thamani, ubora, viwango vya utekelezaji, maboresho au faida ya programu au jukumu lililotekelezwa vitachambuliwa baada ya kila muda maalumu uliopangwa kufika. Tathmini ya miradi itafanyika wakati na baada ya ufuatiliaji wa miradi na ripoti kuandaliwa.

## 5.1 Faida ya ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya ufugaji mifugo kibiashara

Faida ya ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya ufugaji kibiashara ni pamoja na:

i) Kuboresha usimamizi katika kutekeleza viashiria na vigezo vya utekelezaji;
ii) Kurahisisha mapitio ya ufanisi wa kazi (performance review) pamoja na mifumo ya kutoa taarifa na takwimu za tathmini ya kazi;
iii) Kubainisha watekelezaji na mwenendo wa utekelezaji wao;
iv) Kubainisha hatua muhimu za kufuatilia na kutathmini; na
v) Kusaidia kubaini mapungufu mapema kabla ya kupoteza tija na ubora wa kazi na kuchukua hatua stahiki za kurekebisha.

## 5.2 Mambo yatakayozingatiwa wakati wa ufuatiliaji wa miradi ya ufugaji mifugo kibiashara

Timu ya ufuatiliaji wa miradi ya uzalishaji mifugo kibiashara itapaswa kuzingatia yafuatayo:

i) Viashiria vya miradi na majukumu yaliyolengwa;


ii) Kanuni, usalama na tamaduni za mazingira waliyomo wakati wote wanapokuwa uwandani;
iii) Vihatarishi vya miradi vilivyopo na vinavyoweza kujitokeza;
iv) Kupitia kwa kina taarifa za upembuzi wa mwenendo wa hali ya miradi;
v) Kupitia kwa kina taarifa za upembuzi wa mwenendo wa makusanyo ya maduhuli na utendaji wa mifumo ya makusanyo;
vi) Kuzingatia ubora na viwango vya kazi vilivyopangwa na vinavyotarajiwa; na
vii) Uadilifu katika kukusanya vielelezo na maandalizi ya taarifa.


### 5.3 Vielelezo vitakavyotumika kukusanyia taarifa wakati wa ufuatiliaji wa miradi katika Vituo Atamizi

Kwa upande wa miradi ya unenepeshaji wa mifugo, mambo yatakayofuatiliwa ni pamoja na ubora wa mifugo inayonenepeshwa, idadi ya washiriki kwenye vituo atamizi, uwazi wa taarifa za mradi kwa vikundi vya unenepeshaji, hali ya utunzaji taarifa za fedha za mradi, na taarifa za usalama wa mradi.

## 6.0 HITIMISHO

Utekelezaji wa mpango wa ufugaji mifugo wenye tija kupitia Vituo Atamizi unategemewa kuwaandaa vijana kuwa wafugaji kibiashara watakaotumika kuvutia vijana wengi zaidi kuingia kwenye ufugaji wenye tija. Utaratibu huu utasaidia kuongeza fursa za ajira kwa vijana, kukidhi mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi, kuongeza kipato cha kaya na kuongeza mchango wa Sekta ya Mifugo katika pato la taifa. Mwongozo huu wa uendeshaji wa Vituo Atamizi vya ufugaji mifugo kibiashara kwa vijana kwa ushirikiano kati ya Sekta ya Umma na Binafsi utaanza kutumika rasmi mwezi Septemba, 2022.





A
B
C
D
E
F
G
H
56,200
10,000
5,000
1,200
1
2
3
4
5
6
27,000
8,000
4,000
3,000
PEN -1
PEN -2
PEN -3
PEN -4
PEN -5
PEN -6
PEN -7
PEN -8
PEN -9
PEN -10